



Mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo ulioingizwa ndani ya utaratibu wa Mapinduzi ya Kijani umeshindwa kuhakikisha uhakika wa chakula, kuboresha hali ya maisha ya watu wa vijijini na kupunguza umasikini. **BADALA YAKE**, mpango huu umesababisha utegemezi unaotia hofu kwa wakulima wa pembejeo zilizotolewa (mbegu zilizothibitishwa, mbolea na viuatilifu) na kuwalazimisha wao kwenye mtego wa madeni usio na mwisho.

Vocha, mbolea na pembejeo nyingine mara nyingi hupotea au kuibiwa kabla ya kufika kwa wakulima. Wale wakulima wanaozipokea mara nyingi huziua kwa wakulima wenye kipato kikubwa.

Baadhi ya vigezo vya mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo huwaacha waathirika walio wengi – hasa wakulima wanawake ambao pia hutengwa na maafisa wa wilaya na machifu wa vijiji. Makundi haya pia hayamudu kulipa ada ya uwanachama kwa mashirika ya wakulima na michango inayohitajika kufuzu kupata pembejeo.

Mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo hauzisaidii nchi kujenga mifumo imara na endelevu ya kilimo na chakula. Badala yake, inaongeza hali ya kutokuwa na uhakika wa chakula na umasikini, na kuharibu rasilimali za udongo na maji ya Afrika.

Kwanini mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo umeshindwa kufikia malengo yake?

